# CLASS 7 HOLIDAY HOMEWORK TERM 2 2020

## KISWAHILI

### JUMA LA KWANZA - JUMATATU

**A. Toa majibu ya salamu hizi.**

1. Buriani - ____________________
2. Alamsiki - ____________________
3. Lala unono – ____________________
4. Usingizi mwanane - ____________________
5. Sabalkheri - ____________________

**B. Toa maelezo ya maneno haya.**

1. Hayati - ____________________
2. Mheshimiwa - ____________________
3. Omba radhi - ____________________
4. Mtukufu - ____________________
5. Simile - ____________________

### JUMA LA KWANZA - JUMANNE

**A. Andika sauti tata kutokana na herufi hizi.**

1. ( L, r ) - ____________________
2. (j, ch ) - ____________________
3. (f, v) - ____________________
4. (b, p) - ____________________
5. (s, z) - ____________________

**B. Tambuaa matumizi haya ya 'po'.**

1. Painamapo ndipo painukapo.

____________________

2. Tuendapo sipajui.

____________________

3. Alipofaulu alipata zawadi.

____________________

4. Wanionapo hununa.

______________________________

5. Alipozuru Pwani ndipo alipougua.

______________________________

## JUMA LA KWANZA - JUMATANO

**A. Toa visawe vya maneno haya.**

1. Kilimo . - ______________________________
2. Runinga. - ______________________________
3. Kinyonga. - ______________________________
4. Fukara. - ______________________________
5. Kipusa. - ______________________________

**B. Kamilisha kike na kiume.**

| | |
|---|---|
| 1. Koo | ______________ |
| 2. Tembe | ______________ |
| 3. ______________ | fahali. |
| 4. ______________ | mtwana. |
| 5. Hau | ______________ |

## JUMA LA KWANZA - ALHAMISI

**A. Kamilisha vitendawili hivi.**

1. Kutoa ni kuongeza - ______________________
2. Ninacho lakini sikitumii - ______________________
3. Nikigongwa gongwa wanangu hutoka - ______________
4. Nyumbani mwangu hamkosekani unga - ______________
5. Hushinda wakikimbizana - ______________

**B. Toa maana ya emi hizi.**

1. Lia ngoa. - ______________________________
2. Kula mwata. - ______________________________
3. Iva uso. ______________________________
4. Enda nguu. - ______________________________
5. Vika kilemba cha ukoka. - ______________________________

## JUMA LA KWANZA - IJUMAA

**Soma shairi lifuatalo kasha ujibu maswali yafuatayo.**

Jitahidi mwanafunzi, kusoma uendelee.
Sishughulike na penzi, hivi sasa ligomee
Kwani penzi ni kitanzi, nakwambia mwana ee
Wajaitwa mbuzi mee, au uitwe mshenzi.

Aula kwenda sinema, mlani huyo shetani
Sije baki kitetema, au kutemwa shimoni
Shika nasaha ya mama, sijute ulimwenguni
Wajaitwa mbuzi mee, au uitwe mshenzi.

Elimu nguzo muhimu, daraja maisha bora
Wote waliohitimu, wavuna bila hasara
Natangaza ya elimu, yalo bora hata bara
Wajaitwa mbuzi mee, au uitwe mshenzi.

1. Mtunzi wa mashairi huitwa ______________________________
2. Kitabu cha masahairi huitwa ______________________________
3. Shairi hili ni la aina gani ______________________________
4. Taja vina vya kati na vya mwisho katika ubeti wa kwanza.

   ______________________________
5. Taja majina manne yanayoweza kupewa mshororo wa nne katika shairi hili.

   ______________________________
6. Taja mwanzo wa ubeti wa pili. ______________________________

7. Taja utao wa mleo katika ubeti wa tatu. ____________________

8. Ni maudhui yapi yaliyojitokeza katika ubeti wa tatu.

____________________

9. Ni fani gani ya lugha iliyotumika katika ubeti wa kwanza anaposema "penzi ni kitanzi"? ____________________

10. Kanuni za ushairi huitwa ____________________

## JUMA LA PILI - JUMATATU

**A. Andika vitenzi hivi katika hali ya 'o' rejeshi tamati.**

1. Anayekula . ____________________
2. Anayesoma. ____________________
3. Anayekuja. ____________________
4. Anayekataa. ____________________
5. Inayokucha. ____________________

**B. Kanusha sentensi hizi.**

1. Ungeniita ningeitika.

____________________

2. Angalikuja tungalisafiri.

____________________

3. Ukiitwa uitike.

____________________

4. Alikula na kunywa maji.

____________________

5. Kusoma kwake kunavutia.

____________________

## JUMA LA PILI - JUMANNE

**Nyambua vitenzi hivi kama ilivyoagizwa.**

| **Kitenzi** | **kutendesha** | **kutendwa** |
|---|---|---|
| 1. ogopa | __________ | __________ |
| 2. lia | __________ | __________ |
| 3. nata | __________ | __________ |
| 4. soma | __________ | __________ |
| 5. kataa | __________ | __________ |

## JUMA LA PILI - JUMATANO

**A. Tumia viunganishi mwafaka kujazia pengo.**

1. __________ ya kufanya mtihani vyema aliuvurugavuruga.
2. __________ umefika tutaweza kuondoka.
3. __________ nyumba kuwa kubwa haikuwatoshea wageni wote.
4. Naomba __________ shilingi tano ninunue mumunye.
5. Nilimwua simba ________ paka?
6. Unaweza kuishi raha mustarehe __________ uwe na pesa.
7. Wasaliti wale walimwadhibu ______________ ya kosa lolote.
8. Mama alinileteа vibanzi _________ matunda.
9. __________ mimi huoga mara mbili kwa siku.
10. Nitamwita _________ ningependa kumwonya.

## Juma la pili - Alhamisi.

**A.**

1. Taja pambo linalovaliwa shingoni pamoja na mkufu. __________
2. Taja mapamba matatu yanayovaliwa.
   a). Masikioni __________, __________, __________.
   b). Shingoni __________, __________, __________.
   c). Mguuni __________, __________, __________.
   d). Mikononi __________, __________, __________.
3. Usoni mtu anaweza tiwa chale au ______________.

4. Kikuku cha mguuni huitwa ________________.

5. Taja pamba moja la kichwani. ________________

**B. Tambua matumizi ya KWA.**

1. Mama alituandalia wali kwa nyama.

________________

2. Nitaenda kwa arusi ya nyanya yangu.

________________

3. Akinialika nitapitia kwake.

________________

4. Kusoma kwa Kamau kunatisha.

________________

5. Murono alitembea kwa madaha.

________________

## JUMA LA PILI - IJUMAA.

**A. Toa visawe vya methali hizi.**

1. Ngoja ngoja huumiza matumbo.

________________

2. Haraka haraka haina baraka.

________________

3. Mtoto hutazama kisogo cha nina.

________________

4. Si chote king'aacho ni dhahabu.

________________

5. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu.

________________

**B. Toa wingi wa sentensi zifuatazo.**

1. Mtume yule aliletewa mkunga mnene na mkunga yule.

_______________

2. Kungwi huyo ni shemeji yangu.

_______________

3. Ua wa baba una waridi zuri.

_______________

4. Bata hodari amevuka daraja.

_______________

5. Seremala yule alimwua nyani mkongwe.

_______________

## JUMA LA TATU - JUMATATU

**A. Tambua ngeli ya maneno haya.**

1. Mijomba, Nyuni. - _______________
2. Nyenzo, Nyuzi, Nyasi. - _______________
3. Wema , Uovu, Uchizi. - _______________
4. Miwani, Miraa, Mirathi. - _______________
5. Sukari, Chai, Hewa. - _______________

**B. Tambua nomino kundi hizi.**

1. _______________ ya miaka.
2. _______________ la pamba au ugozi.
3. _______________ la mahindi au mtama.
4. _______________ ya ndizi.
5. _______________ cha wachawi.

E-mail: infosnkenya@gmail.com | ORDER ANSWERS ONLINE at www.schoolsnetkenya.com

## JUMA LA TATU - JUMANNE

**A.**

1. Malipo ya kuolewa huitwa ______________________.
2. Malipo kwa ajili ya kutolewa damu ni _______________ au ____________.
3. Malipo ya kwanza shuleni huitwa _________________.
4. Malipo ya kwanza ya bei ya kitu kinachonunuliwa ni _________________.
5. Malipo ya kitu kilichopotea huitwa ______________________.

**B. Msamiati mseto.**

**Toa maana ya :**

1. Mwongo – ______________________________________________
2. Kikwi – ______________________________________________
3. Nambari witiri – ______________________________________________
4. Nambari tasa – ______________________________________________
5. Nambari shufwa – ______________________________________________

## JUMA LA TATU - JUMATANO

**A. Toa maana ya**

1. Kiwanda – ______________________________________________
2. Vipuri – ______________________________________________
3. Fuawe – ______________________________________________
4. Cherehani – ______________________________________________
5. Kusindika – ______________________________________________

**B. Andika sentensi hizi upya kwa kutumia 'amba'.**

1. Ng'ombe aliyeuawa amepikwa.

   ______________________________________________

2. Mkuki uliorushwa ulipotea.

   ______________________________________________

3. Kiatu kilichonunuliwa kilipotea.

   ______________________________________________

4. Ua uliopandwa umekauka.

   ______________________________________________

5. Wema unaozungumziwa ni huu.

   ______________________________________________

## JUMA LA TATU - ALHAMISI

**A. Tumia kiulizi kilicho mabanoni kujazia pengo.**

1. Watoto waliona nyumba ____________________? **(ngapi )**
2. Uliona mijusi ______________________ ? **(ngapi)**
3. Watoto ______________ walifagia daraja ? **(gani )**
4. Msusi alisuka mikeka ____________ ? **(-pi)**
5. Madaraja ____________ yalisombwa na maji ? **(-pi)**

**B. Tumia 'ndi'.**

1. Mimi ________ niliyemwita.
2. Wewe ___________ uliyetumwa.
3. Wao ______ waliotuita.
4. Gunia hilo ________ aliloleta.
5. Hii _________ maana ya kutuita ?

## JUMA LA TATU - IJUMAA

1. Mtu anayesafisha choo na kufagia barabara za miji huitwa __________.
2. ____________ ni mtu mwenye elimu ya nyota.
3. ___________ ni mtu anayefua visu.
4. __________ ni mtu anayetia vitu urembo au nakshi.
5. Toa maana ya ;

   a). Mkiritimba – ______________________________________________

   b). Mhafidhina – ______________________________________________

   c). Mkalimani – ______________________________________________

   d). Hawinde – ______________________________________________

   e). Mualisaji – ______________________________________________

   f). Hamali – ______________________________________________

   g). Kibaraka – ______________________________________________

# JARIBIO LA KWANZA

***Soma vifungu vifuatavyo, vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila pengo umepewa majibu manne. Chagua jawabu lifaalo zaidi.***

Wavyele na washikadau wengine katika ___1___ya elimu ___2___waziwazi kuhusu 3___la kudumisha nidhamu ___4___watoto wa shule. Walimu wanawanyoshea kidole cha 5___ wavyele hasa baada ya ___6___ ya kiboko___7___nchini. Kwa upande wao, wazazi wanajitetea kuwa walimu ndio wa kushutumiwa maadamu wanashinda___8___watoto hawa 9___. Hata hivyo, suala la nidhamu linahusisha kila mmoja katika jamii.

1. A. shirika B. taasisi C. sekta D. kazi
2. A. wamehitilafiana B. wameelewana C. wameulizana D. wamekubaliana
3. A. dhima B. wadhifa C. juhudi D. jukumu
4. A. dhidi ya B. miongoni mwa C. mbali na D. zaidi ya
5. A. lawama B. laana C. baraka D. ushindi
6. A. vita B. adabu C. adhabu D. mapigano
7. A. kupigwa vijembe B. kupigwa dafrau C. kupiga hatua D. kupigwa marufuku
8. A. kwa B. na C. ya D. pa
9. A. mchana kutwa B. usiku kucha C. usiku kutwa D. mchana kucha

Wakazi wengi wa mjini ___10___ na tatizo la uhaba ___11___maji ___12___. Jambo hili hufanya___13___yao kushindwa kuyatunza mazingira yao. ___14___ serikali ichukue hatua ya kusambaza maji kote ili kuepuka kuzuka kwa maradhi kama vile ___15___.

10. A. wamekutwa B. wanakabidhiwa C. wanakabiliwa D. wamejuzwa
11. A. la B. ya C. na D. wa
12. A. masafi B. safi C. swafi D. msafi
13. A. baadhi B. wengi C. wengine D. baina
14. A. Bora tu B. yamkini C. kama D. Ni bora
15. A. pepopunda B. kifaduro C. waba D. surua

***Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.***

16. Tambulisha sentensi yenye tashbihi;
    A. Kaka yake ni msiri kama usiku
    B. Maneno yake yalikuwa msumari moto
    C. Ukitaka kumla nguruwe chagua aliyenona
    D. Kunywa pombe husababisha balaa na beluwa

17. Mfinyanzi ni kwa finyanga kama vile msasi ni kwa
A. msako
B saka
C. msasa
D. usasi

18. Mkungu ni wa ndizi, _____ni kwa funguo.
A. kicha B. jozi
C. bunda D. chane

19. Andika tarakimu 100,001 kwa maneno
A. Laki moja elfu na moja
B. Laki moja na moja elfu
C. Laki mia moja na moja
D. Laki moja na moja

20. Ali**ki**ona kilichomtoa kanga manyoya. Kiambishi **ki** kimetumikaje katika sentensi hii?
A. Kuonyesha masharti
B. Hali ya kuendelea
C. Kama kiwakilishi
D. Kuonyesha udogo

21. Ni sentensi gani yenye kihusishi?
A. Mchezaji yule ni hodari sana
B. Kitoto kimezaliwa chini ya mti
C. Maneno yake yaliniumiza sana
D. Sote tulikimbia mkikimkiki.

22. Majira baina ya saa tisa mchana na magharibi ni
A. alasiri B. adhuhuri
C. mawio D. macheo

23. Tegua kitendawili kifuatacho;
Dhahabu yangu haishuki bei.
A. macho B. almasi
C. shamba D. jiwe mtoni

24. Chagua maelezo sahihi ya viungomwili
A. Taya ni nyama zinazoshikilia meno
B. Kwapa huwa chini ya bega
C. Nyonga huwa juu ya kiuno
D. Kisugudi ni baina ya muundi na wayo

25. Kanusha sentensi ifuatayo kwa usahihi
Mtoto akila sana hunenepa
A. Mtoto asipokula sana hunenepa
B. Mtoto akila sana hanenepi
C. Mtoto akila sana huwa hanenepi
D. Mtoto asipokula sana huwa hanenepi

26. Sentensi gani imetumia **'kwa'** ya umilikaji?
A. Wageni walikuja kwangu jana
B. Sherehe iliandaliwa kwa Maria
C. Bi arusi alikaribishwa kwa vishindo
D. Tulienda moja kwa moja hadi mjini

27. Farasi ni mnyama wa jamii ya punda. Farasi pia ni
A. elimu ya mienendo ya nyota
B. chombo cha kufumia nyuzi
C. anayefuga wanyama wa kupandwa
D. fremu ya baiskeli

28. Shughuli yoyote ikitendwa kupita kiasi huharibika
Chagua methali inayolingana na maelezo haya;
A. Ngoja ngoja huumiza matumbo
B. Ngoma ikilia sana hupasuka kiwambo
C. Tamaa mbele mauti nyuma
D. Chombo cha kuzama hakina usukani

29. Kikembe cha papa huitwaje?
A. Kinengwe B. Kitekli
C. Kiwavi D. Kipura

30. Andika katika usemi wa taarifa;
"Tafadhali niletee miwani yangu nisome gazeti," babu akaniambia
A. Babu alimwambia ampelekee miwani yake asome gazeti
B. Babu aliniagiza nimpe miwani yake asome gazeti
C. Babu aliniomba nimpelekee miwani yake asome gazeti.
D. Babu alimwamuru ampelekee miwani yake asome gazeti.

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 – 40***

Waziri wa Afya nchini Bwana Siha, amesema kuwa huduma za afya nchini zimeimarika kwa kiasi kikubwa katika miaka mitatu iliyopita. Akiwahutubia wananchi waliokuwa **wamejumuika** katika zahanati mpya ya Dawa Mujarabu, Bw. Siha alisema kuwa wizara yake imeongeza zahanati mia tatu katika kipindi hiki kifupi, hasa katika sehemu ambazo wananchi walikuwa wakitembea kwa mwendo mrefu kusaka huduma . Alisema kuwa zahanati nyingi zilizojengwa majuzi zina vifaa vya kutosha kutoa huduma za kimsingi na kukabiliana na magonjwa yanayowataabisha wananchi kama vile malaria na homa ya matumbo. Aliongeza kuwa wizara yake imejenga maabara na kutoa mitambo ya kisasa katika zahanati hizo itakayoweza kutoa uhakika wa magonjwa yanayowasumbua wagonjwa. Alisema kuwa zahanati hizo zina dawa za kutosha.

Aliongeza kuwa wizara yake imeongezea vituo vingi vya afya ili kuwahudumia wananchi. Vituo hivi vina **mitambo iliyo na uwezo wa kupiga picha viungo vya ndani** ili kuweza kutambua magojwa ya ndani kwa ndani yanayowasumbua wananchi. Aliongezea kuwa kila kituo kina wodi ndogo zenye uwezo wa kuwalaza wagojwa takriban thelathini. Hii ni hatua nzuri ikikumbukwa kuwa awali hata kupata dawa ilikuwa shida, jambo lililowapelekea watu wengi kufariki.

Bw.Siha alitoa wito kwa wananchi wajitahidi kuyatunza mazingira. Hali hii itaweza kuwaepusha na magonjwa yanayoweza kuzuilika kama vile malaria na homa ya matumbo. Akitoa vyandarua vilivyotiwa dawa, Bw. Siha alisema kuwa sasa idadi ya watu wanaoambukizwa ugojwa huu imepungua sana katika maeneo mengi humu nchini. Alitoa mwito kwa watu, hasa kina mama wajawazito na watoto walale chini ya vyandarua. Walliougua walihimizwa kutafuta matibabu haraka iwezekanavyo. Aliwakumbusha kuwa matibabu ya malaria sawa na yale ya ugonjwa wa kifua kikuu na UKIMWI hutolewa bure kote nchini. Aliwahimiza wananchi kujua vianzo vya magonjwa mbalimbali ili waweze kujiepusha nayo.

31. Kulingana na waziri wa Afya Bw. Siha
   A. afya imeweza kuimarishwa kote nchini
   B. watu wengi nchini watakuwa wenye afya
   C. matatizo ya kiafya yanashughulikiwa vizuri
   D. serikali itaanza kutoa huduma bora za afya

32. Maana ya "**wamejumuika**" kwa mujibu wa kifungu ni
   A. wamefumukana
   B. wamefungamana
   C. wametandazika
   D. wametengamana

33. Kwa sasa, zahanati zilizopo ni
   A. zaidi ya mia tatu
   B. mia tatu kamili
   C. karibu mia tatu
   D. kama mia tatu

34. Ugonjwa wa malaria husababishwa na nini?
   A. Mbung'o
   B. Maji yaliyotuama
   C. Mbu
   D. Viroboto

35. Malaria na homa ya matumbo
   A. ndiyo maradhi pekee yanayohangaisha wananchi
   B. ni baadhi tu ya shida za wananchi hawa
   C. ni magonjwa yanayowashika watoto
   D. ni magonjwa yasiyotibika kwa urahisi

36. **'Mitambo iliyo na uwezo wa kupiga picha viungo vya ndani,'**hii ni mitambo ipi?
   A. Kamera
   B. Uyoka
   C. Hadubini
   D. Machela

37. Watu wengi walifariki kutokana na
   A. uhaba wa hospitali
   B. ukosefu wa wodi
   C. uhaba wa matibabu
   D. ukosefu wa matibabu

38. Kutunza mazingira ni muhimu kwa kuwa
   A. husaidia kuponya magojwa yawezayo kuzuilika
   B. huzuia kuenea kwa ugojwa wowote ule
   C. hudhibiti kuenea kwa maradhi yawezayo kuzuilika
   D. Ndio njia pekee ya kutunza afya zetu

39. Ni magonjwa mangapi yanayotibiwa bila malipo kwa mujibu wa makala?
   A. Mawili
   B. Matatu
   C. Yote
   D. Manne

40. Kichwa mwafaka kwa makala haya ni
   A. Huduma za afya
   B. Hotuba ya rais
   C. Afya bora
   D. Ugonjwa wa malaria

***Yasome makala yafuatayo kisha ujibu maswali 41 – 50***

Muale **hakuwa mwenda guu**. Aliamua kufanya lolote ambalo lingempa posho ya siku. Akaona bora asibague kazi. Nguo zake zilizochakaa sasa na viatu vyake vilivyokuwa vimepasuka soli vingefaa sana katika kazi nyingine. Akamwendea mwenye mikokoteni mjini kuomba afaliwe, awabebee watu mizigo kisha amlipe jioni. Akaambiwa kuwa katika dunia hii ya nipe nikupe malipo huwa ya asubuhi. Maskini Muale hakuwa na senti zozote. Ilimbidi kuwabebea watu mizigo katika maduka makuu kwa mikono kwa muda akiwapelekea katika vituo vya magari ili apate chochote. Hatimaye aliweza kukusanya za kutosha kukodi rukwama. Msomi mwenzetu akawa hamali.

Alifanya kazi hii kwa moyo wake wote, akawa akirauka alfajiri kuenda kuwapelekea wachuuzi mizigo yao sokoni. Hakusahau kumshukuru Mungu kila uchao kwa hali yake na kumwomba siku njema baadaye. Baada ya siku nyingi za kazi hii ya sulubu, mwenzetu aliweza kujinunulia suti moja na jozi ya viatu akajiwekea nyumbani. Alikuwa na matumaini kuwa siku moja jua la baraka lingemwangazia. Akaendelea kuvaa magwanda ya kazi ya mkokoteni.

Siku moja kilitokea kisa ambacho kilikuwa mchanganyiko wa simanzi na baraka- **wakati mwingine baraka hujia motoni**. Alikuwa ameiburura rukwama yake nzito kwa msaada wa kijana mmoja aliyekuwa akishirikiana naye wakati ambapo mizigo ingekuwa mizito zaidi. Walikuwa wamechoka tiki. Mara likatokea gari moja la kifahari, likakosa mwelekeo, likaugonga mkokoteni na kuwaumiza vibaya. Mwenzetu hakujua lililofuata.

Alipozinduka alijikuta hospitalini baada ya siku kadhaa. Alikuwa kavunjika mguu wa kulia na mkono wa kushoto. Juu ya dawali lake aliziona nakala za vyeti vyake vya chuo kikuu ambavyo daima alivibeba mfukoni. Vilikuwa vimechakazwa na wingi wa damu iliyovimwagikia wakati wa ajali ile. Alimwona msukuma rukwama mwenzake katika kitanda kingine upembeni. Karibu naye pia walikuwa mahamali wenzake waliomzuru kumjulia hali. Pia alikuwepo mtu mmoja aliyeonyesha wazi kuwa ukwasi ulikuwa umemwota si haba.

Mtu yule alimpa pole na kujitambulisha kwake kwamba ndiye aliyemgonga Muale. Ni jambo lililomhuzunisha sana. Ila alikuwa na jingine. Alimhakikishia kuwa angelipwa fidia na shirika lililomkatia bima. Pia alimweleza kuwa yeye alikuwa mkurugenzi wa shirika kubwa zaidi nchini lisilo la kiserikali. Alivichukua vyeti vya Muale na kuvikagua. Akamwomba akaviruduf. Alipovirejesha akajiendea zake na kuahidi kurudi baadaye. Japo alikuwa **akishetasheta**, mkurugenzi yule alikuwa pale na hakikisho. Alitabasamu akamkabidhi barua iliyomwatua moyo kijana yule - yaliyoandikwa yalikuwa ya kuacha kinywa wazi. Alikuwa ameajiriwa tayari kama meneja mkuu wa shirika lile. Hii ndiyo kazi aliyokuwa ameisomea chuoni. Alikuwa aripoti kazini baada ya miezi miwili, muda uliotosha kupona kwake.

41. Muale **hakuwa mwenda guu**, ndiko kusema
A, alikata tamaa
B. hakufa moyo
C. hakutembea kwa miguu
D. alikuwa na masomo ya juu

42. Muale alimwendea mwenye mikokoteni kwa lengo la
A. kuomba kazi ya uhamali
B. kukopeshwa mkokoteni
C. kumweleza matatizo yake aliyopitia
D. kupewa mkokoteni alipie kodi baadaye

43. Anayebeba mizigo kwa rukwama ni hamali ilhali muuza maji ni
A. mzegazega
B. mchuuzi
C. mwanamaji
D. dalali

44. Jambo alilozingatia sana Muale maishani ni
A. kurauka mapema, kujihurumia maishani
B. kuwafaa wengine, kuomba maishani
C. kushukuru kwa hali yake, kuomba neema
D. kuomba asubuhi, kuwashukuru wateja

45. Muale alinunua suti na viatu kwa kuwa
A. alivihitaji wakati asipokuwa kazini
B. alitarajia kuvitumia baada ya kuneemeka
C. alitaka kuwa tofauti na mahamali wengine
D. angevihitaji atakapowatembelea wazazi

46. 'Wakati mwingine baraka hujia motoni,' kifungu hiki kinaeleza kuwa
A. baraka huja matumaini yakiwa hafifu
B. baraka huwaendea waonekanao duni
C. baraka huwafuata wenye imani kubwa
D. baraka huja kwa njia inayodhaniwa kuwa ya tabu

47. Gari lililomgonga Muale lilikuwa
A. shangingi
B. kachara
C. karandinga
D. rukwama

48. Mzee mkwasi alionyesha kuhuzunishwa na
A. hali mbaya ya Muale
B. ajali aliyosababisha
C. damu kwenye vyeti
D. kutomakinika barabarani

49. Mafanikio ya Muale yanaweza kuelezwa na methali kuwa
A. Mgaagaa na upwa hali wali mkavu
B. Dawa ya moto ni moto
C. Mungu akiziba hapa huzibua pale
D. Dau la mnyonge haliendi joshi

50. Maana ya **akishetasheta** kulingana na muktadha ni
A. alitetemeka sana
B. akienda kwa mkongojo kwapani
C. akichechemea
D. akijikokota

# JARIBIO LA PILI

***Soma vifungu vifuatavyo, vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila pengo umepewa majibu manne. Chagua jawabu lifaalo zaidi.***

Kazi ya ___1___ vyuma hufanywa na ___2___. Hii ni mojawapo ya kazi za ___3___ maadamu huhitaji nguvu nyingi kuitekeleza. Wanaotaka kujifunza kazi hii huhitajika kupiga kambi na ___4___ kwa muda ili kujipatia maarifa. ___5___, hawana budi kuwa na uvumilivu kwani ___6___. Hatimaye, baada ya kuhitimu ___7___ mafunzo yao, wao hutafuta ___8___ na kujianzishia karakana ___9___ wenyewe.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. kuvua | B. kufua | C. kuvunja | D. kuunda |
| 2. | A. mwashi | B. sonara | C. dobi | D. mhunzi |
| 3. | A. shokoa | B. ujima | C. sulubu | D. kijungujiko |
| 4. | A. wajuzi | B. wajuaji | C. mijusi | D. mijuzi |
| 5. | A. Hata hivyo | B. Ama | C. Pia | D. Ingawa |
| 6. | A. kiingiacho mjini si haramu | B. mstahimilivu hula mbivu | C. chelewa chelewa utapata mana si wako | D. jungu kuu halikosi ukoko |
| 7. | A. ya | B. ndani ya | C. kwa | D. katika |
| 8. | A. mtaji | B. arbuni | C. ridhaa | D. koto |
| 9. | A. mwao | B. wao | C. zao | D. vyao |

Baada ya mashindano yale, walimu na wanafunzi wenzangu walianza ___10___ na mtazamo tofauti ___11___. Nilikuwa nimejinyakulia ___12___ nishani zote ___13___ siku ile. Ingawa ___14___ yangu shuleni hayakuwa ya kutia moyo sana, kipawa changu katika riadha kilikuwa ___15___ wazi sasa.

| | A | B | C | D |
|---|---|---|---|---|
| 10. | A. kua | B. kuwa | C. kukuwa | D. kwa |
| 11. | A. yangu | B. nami | C. kwao | D. kwangu |
| 12. | A. kama | B. nusura | C. takriban | D. karibia |
| 13. | A. zilioshindaniwa | B. zilizoshinda | C. zililoshindaniwa | D. zilizoshindaniwa |
| 14. | A. maendeleo | B. maendelezo | C. mwendeleo | D. mwelekeo |
| 15. | A. kimedhihirishwa | B. kimedhihirika | C. kimeathirika | D. kimethihirishwa |

***Kuanzia nambari 16 mpaka 30, jibu kila swali kulingana na maagizo uliyopewa.***

16. Sentenzi gani imetumia 'ni' kuonyesha wingi?
    A. Mizigo yenyewe ni mizito sana
    B. Panya wote wamejificha shimoni
    C. Zingatieni ushauri wote mliopewa
    D. Nilimpelekea bidhaa zote alizoagizia

17. Kipi ni kielezi katika sentensi ifuatayo?
Ng'ombe wake mnono alivunjikia mguu malishoni
A. mnono B. wake
C. malishoni D. alivunjika

18. "*Ukiona ndugu wawili wakipigana chukua jembe ukalime*"
Kipi ni kisawe cha methali hii?
A. Meno ya mbwa hayaumani
B. Kikulacho ki nguoni mwako
C. Kidole kimoja hakivunji chawa
D. Adhabu ya kaburi aijuaye maiti

19. Kamilisha kwa tanakali ifaayo zaidi. Baada ya ajali, gari lake
A. lilichanika chanechane
B. lilibatana batabata
C. lilikauka kukutu
D. lilipekua pekupeku


20. Ugonjwa wa mishipa ya fahamu unaosababisha viungo vya mwili kukatikakatika ni
A. pepopunda B. surua
C. machapwi D. ukoma

21. Bainisha orodha yenye vihusishi pekee.
A. tena, kando ya, sawasawa, zaidi ya
B. baada,tena, kando, pale
C. katika, kwenye, karibu na, pembeni mwa
D. vibaya, alasiri, mbio, dhahiri

22. Andika umoja wa sentensi ifuatayo.
*Malezi tuliyopewa yametufaa sana*
A. Malezi niliyopewa yametufaa sana
B. Ulezi niliopewa umenifaa sana
C. Ulezi aliopewa umefaa sana
D. Malezi aliyopewa yamemfaa sana

23. Saa 8:45 kwa maneno ni
A. Saa tatu kasorobo
B. Saa tisa kasorobo
C. Saa nane kasorobo
D. Saa mbili kasorobo

24. Taja majina ya vifaa vifuatavyo



A. bisibisi, keekee
B. patasi, timazi
C. pimamaji, jiriwa
D. patasi, jiriwa

25. Konsonanti za Kiswahili ni ngapi kwa jumla?
A. Ishirini na moja
B. Tano
C. Ishirini na tano
D. thelathini

26. Msafiri ni kwa safari kama ilivyo mcheshi kwa
A. cheshi B. kicheko
C. cheka D. chekesha

27. Chagua maelezo sahihi.
A. Vina ni idadi ya silabi za mishororo
B. Mizani ni silabi zina zofanana katika ubeti
C. Guni ni shairi lenye mishororo minne
D. Mghani huiba mashairi yaliyotungwa

28. *Tuliishangilia timu yetu kwa nguvu sana*
Eleza matumizi ya 'kwa' katika sentensi hii
A. kuonyesha sababu
B. kuonyesha namna ya kutenda
C. kuonyesha mfululizo wa matukio
D. kuonyesha umilikaji

29. Sentensi ipi imetumia kirejeshi 'o' tamati?
A. Lisemalo ndilo liwalo
B. Anayecheka huwa na furaha
C. Tulipochoka tulielekea chengoni
D. Moto unaowaka ni mpishi

30. Kata ni eneo la utawala kata pia ni
A. kutokubali jambo
B. kitambaa cha kufungia jeraha
C. Nyuzi zinazotokana na mkonge
D. Kifaa cha kukorogea mchuzi

***Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 – 46***

Katika maisha yetu ya kila siku, tunaitumia lugha kwa njia moja au nyingine tangu tuamkapo hadi tulalapo. Hata hivyo, si wengi wetu wanaojishughulisha na kuchunguza kwa undani maana na wajibu wa lugha katika maisha yetu. Tunakichukulia kuwa ni kitu cha kimaumbile tu kama ilivyo milima, mito, misitu na kadhalika. Lakini tukitua kidogo na kujiuliza maisha yangalikuwa namna gani iwapo tusingalikuwa na lugha ndipo tunapoweza kuelewa dhima au umuhimu wa lugha katika maisha yetu.

Lugha hutekeleza wajibu muhimu sana katika jamii kwa hakika ni vigumu kufikiria namna maisha yanavyoweza kuwa iwapo binadamu asingekuwa na lugha. Tukijaribu kuwazia shughuli zote tunazotenda kila siku. Tukitumia lugha, basi tunaweza kupata mwangaza tosha kuhusu umuhimu wa lugha katika maisha yetu.

Maisha bila lugha yangekuwa yamejaa **<u>mashaka</u>** matupu yangekuwa yamezungukwa na migogoro, migongano, kutoelewana, dhiki, mafarakano, na mengine mengi yasiyokuwa na faida hata chembe. Ni kwa kupitia lugha tunapoweza kushirikiana na kuwasiliana kwa mema au mabaya. Shughuli zote katika ulimwengu huu tunamoishi - mazuri na mabaya, migogoro na hata vita hutatuliwa kwa kutumia lugha.

Vilevile, binadamu hawezi kuyaelewa mazingira yake asipokuwa na lugha. Ni muhimu kwa binadamu kuyaelewa mazingira yake ili aweze kuyapanga kwa utaratibu unaofaa na kuyapambanua vilivyo. Kwa mfano katika mazingira yetu kunayo miti mimea mingine mbalimbali. Tunahitaji kuipa miti na mimea hii majina, iwe ni miembe,mipera, mikarafuu, mihogo na mingineyo. Kunao pia wanyama ambao tunahitaji kuwabainisha kwa maneno, wawe ni ng'ombe, nguruwe, nyati,nyoka nyangumi na wengine wengi. Miongoni mwa wadudu tuna sisimizi, viroboto, viwavi, panzi, vipepeo na wengine. Je, bila lugha tungewaitaje?

Zaidi ya vitu hivyo, kuna vingine chungu nzima ambavyo vinahitaji kubuniwa majina kama vile samaki, vyombo mbalimbali vya ukulima upishi au jikoni; rangi mbalimbali, nyakati za siku, sehemu za mwili, vifaa vya dukani, ndege, mavazi, vyakula, afya na usafi, magonjwa, maumbo, matunda, mapambo, siku na miezi, dawa, vyombo vya sayansi na teknolojia na vingine vingi. Tunahitaji lugha ili kubainisha vitu hivyo vyote.

Aidha, maendeleo ya nchi zetu yangeathirika mno. Maendeleo hutokana na mawasiliano ambayo huwapa watu uwezo wa kubadilishana mawazo. Kwa njia hii watu huanzisha miradi mbalimbali na kuinua uchumi wao binafsi wa jamii na wa nchi zao kwa jumla. Bila lugha ushirikiano kama huu usingewezekana kati ya watu binafsi au hata kati ya nchi na nyingine kwani unategemea mawasiliano ya kimazungumzo ya moja kwa moja au kwa maandishi. Isitoshe, lugha ndicho chombo cha kimsingi katika kuendeleza taaluma nyingi.

31. Kulingana na aya ya kwanza
    - A. binadamu hawezi kuishi bila lugha
    - B. maisha ya binadamu ni magumu bila lugha
    - C. binadamu angeishi kwa tabu bila lugha
    - D. lugha hufanya maisha kuwa ya tabu

32. Maelezo yapi ni sahihi?
    - A. Kila mmoja huzingatia umuhimu wa lugha
    - B. wachache tu huchunguza dhima ya lugha
    - C. wengi wetu hujishughulisha kuchunguza za dhima ya lugha
    - D. hakuna anayeshughulikia umuhimu wa lugha

33. Ni vigumu kufikiria namna ambavyo maisha yangekuwa bila lugha kwa kuwa
    - A. yangekuwa magumu kipindukia
    - B. akili haziwezi kuyawazia hayo
    - C. wanyama huishi bila kuwasiliana
    - D. binadamu na wanyama hawawezi kuwapo

34. Neno **<u>mashaka</u>** kama lilivyotumika lina maana ya
    - A. hofu
    - B. wasiwasi
    - C. furaha
    - D. dhiki

35. Lugha inapotumiwa kusuluhisha migogoro, basi huwa imeleta
A. maelewano
B. mafarakano
C. mtafaruku
D. chuki

36. Kati ya mimea iliyotajwa, upi hutumika kama kiungo cha mapishi?
A. Mpera
B. Mkarafuu
C. Mihogo
D. Hakuna

37. Binadamu anahitaji lugha katika mazingira ili aweze
A. kuyapamba na kuyapambanua
B. kuyapanga na kuyapangua
C. kuyapanga na kuyapambanua
D. kuyapamba na kuyapambua

38. Lugha inayounganisha wananchi wa makabila mbalimbali katika mawasiliano ya kila siku ni
A. lugha ya kitaifa
B. lugha rasmi
C. lugha ya mama
D. lugha ya taifa

39. Binadamu hutumia lugha kujiendeleza kwa namna zote hizi ila
A. kiuchumi
B. kitaalamu
C. kiteknolojia
D. ubinafsi

40. Kichwa kifaacho zaidi kwa makala haya ni
A. lugha mbalimbali
B. manufaa ya lugha
C. maisha bila lugha
D. lugha za kisasa

***<u>Yasome makala yafuatayo kisha ujibu maswali</u>* 41 – 50**

Ajabu ya ajabu barua za walioachishwa kazi zilipotolewa, Mama Riziki alikuwa mmoja wao. Alishangaa. Wenzake walipozisikia habari zile walishtuka sana. "Iweje na alivyo na juhudi kubwa?," walilalamika. Lakini hamna aliyesikia kilio hicho. Waliosikika wakinung'unika waliulizwa" Mnataka mpigwe kalamu nyinyi?". Wakafyata mikia na kumwachia Mama Riziki zigo lake pekee. Akaondoka kwa huzuni nyingi na malipo ya shilingi elfu arubaini kuelekea kwao nyumbani.

Alipofika nyumbani **<u>hakujikalia kibwete</u>** tu. Aliamua kutafuta la kufanya. Akaanzisha biashara ndogo ya kioski kwa bahati nzuri maskani yake hayakuwa mbali na bwawa. Aliamua kuanza kupanda mboga za kila aina ambazo angeuza kwenye soko la karibu. Juhudi zake zilizaa matunda na baada ya muda akawa akisambaza mboga kwa wingi sokoni.Ile kioski yake sasa ilipanuka, akaongeza mtaji na kuipanua kuwa duka dogo.

Kutokana na biashara yake hiyo aliweza kumudu kuwalipia wanawe karo ya shule pamoja na kuyakidhi mahitaji yao mengine. Wakati wa likizo nao walikuwa tayari kumsaidia mama yao. Siku moja mradi mkubwa wa ujenzi ulianzishwa kwenye soko la karibu. Mama Riziki aliamua kujitosa kwenye uuzaji wa chakula au kapile kwa wale vibarua waliofanya kazi pale. Alipika chapati, kaimati na vyakula vingine huko nyumbani na kwenda kuwauzia. Wengi walikipenda chakula chake kutokana na sababu kadhaa; usafi wake, upishi stadi na uchangamfu na ubinadamu wa mwuzaji aliyekuwa radhi hata kuwakopesha.

Lakini biashara hii mpya ilimzulia matatizo mengine. Pale sokoni palikuwa na wenye hoteli mbili ambao walichukizwa na biashara yake. Walihisi kuwa aliwavuta wateja wao kama nyuki anavyovutwa na mbelewele ya maua. Biashara zao zilianza kukumbwa na matatizo. Walimtishia kumshtaki kwa kufanya biashara bila idhini. Lakini hapo walinoa. Alikuwa tayari keshanunua leseni yakumruhusu kuifanya biashara hiyo.

Wafanya biashara hao waliamua kumlia njama. Alipokwenda kupata leseni baada ya mwaka, alikumbwa na matatizo mapya. Serikali imepiga marufuku uuzaji wa chakula kisichopimwa

na wataalamu" Jamaa aliyehusika alimwambia . Hata hivyo, wale vibarua baada ya kugundua njama iliyokuwako waliamua kuzisusia hoteli zenyewe.

Watu waliungana na kuanza kumpigania mama Riziki. Muda mfupi baadaye aliidhinishwa kuendelea na biashara yake. "Jitihada haiodoi kudura", alijisemea mama Riziki.

41. Watu walizipokea habari za kuachishwa kazi kwa mama Riziki kwa mshangao kwa kuwa
A. alikuwa mwenye bidii kazini
B. alipendwa na wote kazini
C. hakupendwa na watu kazini
D. alikuwa mzembe kazini.

42. Waliolalamikia kufutwa kwake walinyamaza kwa
A. kuelezwa sababu za kufutwa kwake
B. kufahamishwa kuwa alilipwa pesa
C. kutishiwa kuachishwa kazi pia
D. kutulizwa na mama Riziki mwenyewe.

43. Maana ya '**hakujikalia kibwete**' ni kuwa
A. alikaa bila kufanya lolote
B. alikuwa amechanganyikiwa
C. hakupandwa na hasira
D. hakukaa bila kufanya jambo

44. Sehemu inayopandwa mboga karibu na nyumba ni
A. chalo
B. bustani
C. konde
D. jaluba

45. Bishara ya **mboga** ilimsaidiaje mama Riziki?
A. Kuwapeleka wana shuleni na kuwalisha
B. Kukidhi mahitaji ya wana na kuwalipia karo
C. Kukidhi mahitaji yake na kuwaelimisha wana
D. Kuanzisha kioski na kuikimu familia.

46. Watoto wana jukumu gani kulingana na makala?
A. Kusoma kwa bidii na kuanzisha biashara
B. Kuwatafutia wazazi msaada wanapoachishwa kazi
C. Kuwasaidia wazazi kazi wakati wote
D. Kuwasaidia wavyele kazi inapotokea nafasi.

47. Wenye hoteli walimchukia mama Rizika kwa kuwa
A. waliogopa ushindani
B. chakula chao kilikuwa kibovu
C. vibarua wote walihama kwao
D. hawakujua kupika vizuri

48. Wateja walipendelea kwa mama Riziki kwa sababu zote hizi ila
A. unadhifu wake
B. uhodari wa kupika
C. ukubwa wa biashara yake
D. utu wake kwa wateja.

49. Wenye hoteli walikula njama gani?
A. Kumzuilia mama Riziki apate kibali cha biashara
B. Kuwazuilia wateja wasiende kwa mama Riziki.
C. Kumshitaki mama Riziki kwa kutokuwa na kibali.
D. kuboresha bidhaa zao kushinda za mama Riziki

50. Jitihada haiondoi kudura kwa kuwa
A. Wateja walimpigania mama Riziki akafanikiwa.
B. watoto wa mama Riziki waliendelea na masomo
C. Serikali ilimpa mama Riziki leseni bila pingamizi
D. Wenye hoteli walishindwa kuzuia biashara ya mama Riziki.